**JAMHURIYAMUUNGANOWATANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALAZAMIKOANASERIKALIZAMITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NKASI KATIKA MKOA WA RUKWA

**JAMHURIYAMUUNGANOWATANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**MkuuwaShule: 0756781097**
**MakamuMkuuwaShule:0755325878**
**Matron: 0768174416**
**Patron:0763241142**

**ShuleyaSekondari NKASI**
**S.L.P119, Namanyere-Nkasi**
**Tarehe.....................……………**

**Mzazi/MleziwaMwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P……………………………………..**
**…………………………………………….**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NKASI HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI MKOA RUKWA**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2025/2026 na atasoma tahasusi ya **HGL, HGK, CBG, PCB, PMCs** &**PCM**.

Shule ya Sekondari NKASI ipo umbali wa Kilometa 100 Kusini Magharibi mwa Mji wa Sumbawanga.Usafiri wa basi kutoka mjini Sumbawanga unapatikana katika kituo cha mabasi Sokomatola Nauli ni Shilingi 7,000/=. Au katumba standi kuu ukitokea njia ya tunduma

Muhula wa Masomo unaanza tarehe**………….**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **………….** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **……………….**.

**2. Mambomuhimuyakuzingatia:-**

**SarezaShule**

i. Sare ya shule hii ni DAMU YA MZEE NA NYEUSI kwa Wasichana na Wavulana (*Moja kwa kila rangi*). Maelezo ya mshono, sketi ndefu kufunika kisigino (*ambatisha kipande cha kitambaa na picha ya mshono);*
ii. Mashati meupe mikono mirefu (*mawili*);
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni NYEUPE ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama (*mshono upo nyuma ya fomu hii)*
iv. Sare ya Michezo ni truck suit ya blue na T-Shirt ya blue tu. Kwa wasichana na wavulana (*Pair moja*);
v. Viatu vya shuleni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi jozi mbili nyeupe / nyeusi za shule;
vii. Mkanda mweusi wangozi wakuvalia suruali;
viii. Sweta BLUE (*ShingoyaV*);
ix. Nguo za kushindia (*shamba dress*) GAUNI YA BLUE kwa wasichana na Suruali ya DARK BLUE kwa wavulana na T-Shirt ya blue( kwa atakae hitaji yenye nembo ya shule itapatikana shuleni kwa Tsh 15,000/=)
x. Tai NYEUSI na DAMU YA MZEE(Tai ndefu);

**Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari7 au10 (*Qr3 au 4*);
ii. **Ream(A4)** ya Karatasi moja(1)kwa nusu mhula
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika(*orodha iambatishwe*);
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanao soma Biology;
v. Scientific Calculator;
vi. Godoro kwa wanafunzi futi 2½"jipya lenye foronya
vii. Mashuka Jozi 2(Pink na Blue),blanket1,foronyaya godoro1,chandarua 1.
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe) ( haruhusiwi kutumia chombo cha mtu mwingine)
x. Ndoo2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
**xi. Kama hana bima ya afya ya mzazi au mlezi aje na fedha kiasi chaTsh 50,400/= kwa ajili ya Bima ya Afya**

**2.3 VIFAA**

| NA | TAHASUSI | AINAYA KIFAA |
|---|---|---|
| **01** | **PCB** | Kwanjamoja,jembelenyempinimoja,fagioyandani(softbloom)mojana, fagiolanje(la chelewa) mojanamopaya rubber(squizer) |
| **02** | **CBG** | Kwanjamoja,jembelenyempinimoja,fagioyandani(softbloom)moja, fagiolanje(la chelewa)mojanandookubwamoja |
| **03** | **HGL** | Kwanjamoja,jembelenyempinimoja,fagioyandani(softbloom)moja, fagiolanje(la chelewa) mojanamopamojayarubber(squizer) |
| **04** | **HGK** | Kwanjamoja,jembelenyempinimoja,fagioyandani(softbloom)moja, fagiolanje(la chelewa) mojanamopayarubber(squizer) |
| **05** | **PMCs** | Kwanjamoja,jembelenyempinimoja,fagioyandani(softbloom)moja, fagiolanje(la chelewa) mojanahardbloom moja |
| **06** | **PCM** | Kwanjamoja,jembelenyempinimoja,fagioyandani(softbloom)mojana, fagiolanje(la chelewa)mojanareki lenyempini moja |
| **07** | **WOTE** | Sabuni ya maji aina ya Aro toilet cleaner 1000m (1) |

**Michango mbalimbali**

**a)Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | MchangowaUendeshajiwaShule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | KitambulishochaShule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Michango hii iwekwe katika Akaunti Na. 62001100007 NMB JINA LA AKAUNTI NI NKASI SECONDARY SCHOOL**

**Njoo na Bank Pay In Slip.**

**3. SherianaKanunimuhimuzaShule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwakwaSheria Na.10 yamwaka1995.Aidha,inazingatiamiongozo yoteinayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenyejukumu lausimamizi nauendeshaji waelimu nchini. Unatakiwakuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

Sheria na kanuni za shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwaujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba yashule;
iii. Kushirikikwakikamilifumasomo ya usiku(Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli zashuleutakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani nanje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunzausafiwamwili,mavazi namazingirayashule;
vii. Kuvaasareyashulewakatiwoteunapotakiwa;
viii. Kuzingatiaratibayashulewakati wote;
ix. Kutunzamaliza shule;
x. Nimarufukumwanafunzikumilikivifaavyenyenchakalinadawabilaidhiniya daktari; na
xi. Mwanafunziharuhusiwikubadilidiniwalakumshawishimwanafunzimwenzakekubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi ( akija na simu atarudishwa nyumbani ilia arudishe simu hiyo)

- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa.Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).(akiondoka bila ruhusa amejiondoa shule mwenyewe)

**Makosa ya akayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa Zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana na mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kufuga ndevu;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sharia za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera yaTaifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua,au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. ViambatishonaFomuMuhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form)ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomuyamzazikukirikukubaliananasheria,kanuninamaelekezomengineyanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhalisomakwamakini maelezo/maagizohayanakuyatekelezakikamilifu.

**KARIBUSANA KATIKASHULEHII**

**Saini**

**MkuuwaShule:AMIANIEJ.MANGA Mhuri**

**wa Mkuu wa Shule:** THE HEADMASTER NKASI SECONDARY SCHOOL

**NB:Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuuwashule 0756781097 / 0787 262133**
- **MakamuMkuuwaShule 0755325878**
- **MwandamiziTaaluma 0769439651**
- **MwandamiziMalezi 0752 008 126**

***HAKIKISHA FOMU HII UNAKUJA NAYO SHULENI***

**RANGI NA MSHONO WA SARE ZA SHULE KATIKA PICHA**

1 SKETI RANGI DAMU YA MZEE



2 SKETI RANGI NYEUSI, HIJAB

2.SURUALI & SHATI



4.SHAMBA DRESS





***JAMHURIYAMUUNGANOWATANZANIAOFISI YA***
***RAIS - TAMISEMI***
***SHULE YA SEKONDARI NKASI***

## ***FOMUYAKUTHIBITISHAAFYA.***

*(Fomuhiiinajazwanamgangamkuuwahospitaliyaserikali nakurudishwakwamkuuwashuleyasekondari NKASI*

*Jinala mwanafunzi............................................................................*

*Tafadharinaombakwambauwezekumpimahaliyakeyaafyamwanafunzimwenyejinahapojuuili kumthibitishakiasi chakecha afyakuwezakumdushughulizamasomo darasani,kazizamikonona michezo.Tafadhariwekaalamayave(√)mbeleyaeneo alilopimwa/kuchunguzwakwenyeneonHAPANA auNDIYOnaiwaponiNDIYOkwambalimeoonekanatatizobasieleza katikanafasiiliyowekwa.*

*Je,mwanafunzianatatizolololotekatikasehemu zifuatazo?*

1. *Uwezowa kuona:MACHO HAPANA.............NDIYO............ .............*
2. *Uwezowakusikia HAPANA.............NDIYO............ .............*
3. *Uwezowakusema:sauti HAPANA.............NDIYO............ .............*
4. *KifuakikuuTB HAPANA.............NDIYO............ .............*
5. *Shinikizoladamu HAPANA.............NDIYO............ .............*
6. *Ulemavuwaviungo HAPANA.............NDIYO............ .............*
7. *Tatizololote lakiafya HAPANA.............NDIYO............ .............*
8. *AkubaliwekupokelewakusomaHAPANA...........NDIYO............ .............*
9. *Kundilakeladamuni ..........................................................................*
10. *Malalamikomengineyoyoteanayotoamwanafuzikuhusuafya auviungovyake*

    *.......................................................................................................................................................*
11. *Kunatatizoauugonjwakuhusiananaafyayakelinalowezakufanyamwanafunzihuyualazimie kusomashuleiliyokaribunahospitaliyawilayaaumkoa?*

    *..................................................................................................................................................*
12. *Maoninamapendekezoyadaktariapokeleweauasipokelewekuendeleanamasomoyashuleya sekondarimwakaHuu:*

    *......................................................................................................................*

*…………………………… …………………………. ……………………*

*JinakamililaMganga sahihiyako Cheo*

***................................ .................***

***TAREHE MUHURI***